

Ukweli Hauna Kutu

# Pambazuko

Toleo Namba 017

Jumatatu Oktoba 31-Novemba 6, 2022

**Waziri gani anakosa usingizi? Uk.2**

**Rostam  
kanena,  
kamari  
ni janga  
Uk.9**

**Tanzania  
kidedea  
mashindano  
ya dunia  
Uk.14**



*Jacqueline Ntuyabaliwe*

**Jacqueline  
Mengi anyimwa  
milioni 695/-**

● *Adai ni malimbikizo ya matunzo ya watoto*

**JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure**

## **Waziri gani anakosa usingizi?**

**T**UMEKUWA tukiambiwa kwamba Rais Samia Suluhu Hassan anakosa usingizi kwa kuwa anawaza na kuwazua afanye nini ili kupunguza madhila ya wananchi anaowaongoza – Watanzania.

Inawezekana kuna ukweli wa maneno hayo yanayotoka kwa wasaidizi wake, ingawa inaleta ukakasi kidogo kwa kuwa yanatolewa na wanasiasa wetu ambao tunawafahamu hulka na mienendo yao; kupenda kujipendekeza na mara nyingi kusema uongo.

Imani ya wengi ni kwamba kuna asilimia kadhaa ya ukweli kwenye maneno hayo kutokana na ukubwa na ugumu wa kazi ya kuongoza wananchi wengi masikini - idadi kubwa wakikosa kujua watakula nini kwa mlo unaofuata, baada ya kubahatisha mmoja kwa shida.

Pamoja na imani hiyo kwa Rais Samia, hatuna uhakika endapo kuna waziri hata mmoja, anayekosa lepe la usingizi kwa kuwahurumia Watanzania.

Mawaziri wengi tunawaona wakipuyanga tu na kujifanya wako “bize” kutumikia wananchi, lakini matokeo yake hatuyaoni.

Madhila mengi katika wizara yapo kwa kuwa mawaziri hawawajibiki ipasavyo. Kwamba hawafanyi kazi zao kwa ufasaha, hawatumii muda na uwezo wao wa kufikiri kutatua kero lukuki za wananchi.

Hivi sasa maeneo mengi ya Tanzania tunashuhudia- baada ya miaka 60 ya uhuru, bado kuna shida kubwa ya maji, licha ya kuwa na vyanzo vingi vya kupatikana kwa maji, tena kwa gharama nafuu zaidi.

Maeneo mengi ya vijijini yana hali mbaya zaidi kwa kukosa maji safi na salama, hivyo binadamu kulazimika kutumia maji yanayoogeshwa na ama kunyweshwa wanyama. Hii ni aibu kubwa.

Mbali na vijijini, maeneo mengi ya mijini na hata majiji, bado kuna shida kubwa ya maji. Wananchi wanalazimika kutumia fedha nyingi kununua maji kutoka kwa wafanyabiashara wanaouza maji bei aghali mno - kwa kuwa wanatambua hakuna mbadala.

Kwamba hata katika Jiji la Dar es Salaam, lenye kubeba sura ya Tanzania kwa muda wa wiki mbili sasa linakabiliwa na ukosefu wa maji, bila serikali, kupitia kwa waziri husika, kutoa maelezo yanayoeleweka juu ya kadhia hiyo.

Maelezo yanayotolewa na serikali yanaonekana kujaa siasa zaidi kuliko uhalisia. Hivi nini kinashindikana kuwa na vyanzo vya uhakika wakati vipo na kwamba vinahitaji utashi tu na ukosefu wa maji katika maeneo mengi ya Tanzania itakuwa historia!

Inavyoonekana viongozi wengi, hasa wasaidizi wa Rais Samia (kama ilivyokuwa kwa marais wengi waliotangulia) hawana uchungu na madhila mengi yanayowakabili wananchi. Wao wakiteuliwa na kuapishwa, basi kazi kwao imeisha, na wananchi “watajiju.”

Ufike wakati sasa mawaziri na wasaidizi wengine wa rais wawekewe namna nzuri na yenye uwazi, kupima utendaji wa majukumu yao na wakishindwa waondolewe haraka.



## Jisajili kupata Pambazuko bure

Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno “**HABARI**” kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

Pia unaweza kujisajili kwa kutumia Email hii: [pambazuko1@protonmail.com](mailto:pambazuko1@protonmail.com) ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno “**HABARI**” na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

## NUKUU



Taifa hili tumeonewa sana, haiwezekani wao (wazungu) wawe wanachukua chukua tu mali zetu, sisi tunaangalia. Narudia kuwaambieni hivi ndugu zangu, Tanzania ni tajiri – **John Magufuli, aliyekuwa rais wa awamu ya tano. Magufuli sasa ni marehemu.**

---

**Tujadili ripoti siyo wanaojadili ripoti****Na Askofu Dkt. Benson BAGONZA**

**I**JUMAA ya Oktoba 21, Rais Samia Suluhu Hassan alipokea ripoti ya kikosi kazi cha kupitia maoni ya wadau wa demokrasia na kuelezea maoni ya wananchi iliyokusanya na mapendekezo.

Baada ya Rais Samia kupokea ripoti na kuzungumza mtazamo wake, wananchi walisomeka kupitia mitandao ya kijamii na vyombo vya habari, wakijadili ripoti hiyo kwa mitazamo mbalimbali.

Hata hivyo, katika mijadala hiyo ya wananchi, kuna kitu kimoja kikubwa kilijitokeza; kwamba wengi walishindwa kujadili maudhui ya ripoti na badala yake wakajikita kupingana wao kwa wao – yaani hao wanaojadili.

Hali hii ildhihirisha kitu kikubwa kwamba kukosekana kwa midahalo shuleni kumeleta udhaifu wa kujadili masuala katika makusanyiko vijiwani, vyama vya siasa, misibani hata mahakaluni.

Kilichokuwa kikisomeka ni sawa na watu kuacha kujadili nyumba inayoungua moto, na wakajikita kuzungumzia panya na mijusi inayokimbia moto huo! Hii ni ajabu na ni hatari kubwa kwa ustawi wa Tanzania yenye watu wanaoweza kuchambua na kutafakari kwa usahihi yanayoletwa na viongozi au matukio muhimu.

Kwenye mijadala ya ripoti ya Kikosi Kazi (KK) kuhusu masuala ya demokrasia hapa nchini kumeonekana kuwepo kwa kundi linapinga ripoti hiyo.

Lakini pia, limeibuka kundi jingine linapinga kundi linalopinga ripoti hiyo.

Kwa mtazamo wangu, nilidhani tungejadili zaidi uzuri na ubaya wa ripoti hiyo.

Kwamba tusijadili wanaounga mkono au wanaopinga ripoti hiyo.

Kikosi Kazi kimemaliza kazi yake. Aliyepewa ripoti ndiye mwenye dhamana ya kujibu, kutekeleza au kuweka kabatini ripoti hiyo.

*Rais Samia*

Tusiendelee kuipa likizo katiba ya nchi kwa sababu yoyote. Katiba yetu, mbovu au nzuri ituongoze.

Tunasutwa na historia. Tulifikaje hapa? Waliotufikisha hapa, waliosema, na waliokaa kimya, tuna deni kwa taifa letu. Hatuko salama bado.

Tukikosea kanuni za kujadili mambo ya msingi, tunarahisisha uwezekano wa kurudi tulikotoka.

Tuache mizaha, hakuna aliyekuwa salama na hakuna atakayekuwa salama tukirudi huko.

Tumetegemea sana watu wenye nguvu na hatukufika popote. Tujaribu kutegemea taasisi na mifumo imara. Ubinafsi, udini, ukanda, ukabila, uchawa, u-bara, u-zanzibara, uchama-tawala, upinzani, na upinzani wa upinzani tumevipa nguvu kwa hasara yetu wenyewe.

Hakuna tumbo lishibalo milele, ndo maana kuna choo.

**Zinduka.**

---

## Watu wasizibwe midomo

### Na Bullet RUHINDA

**K**AMA Mungu anatoa nafasi ya watu kujieleza sisi ni akina nani kuwazuia wenzetu?

Kwa wasomaji wa Kitabu kitakatifu cha Biblia watakuwa wanaikumbuka hadithi ya wazee wetu; Adam na Eva kufukuzwa kutoka bustani ya Eden.

Katika kitabu cha Mwanzo, sura ya 3 aya ya 11, Mungu anamuuliza Adamu - "je, umekula matunda ya mti niliokuamuru usile?" Nini maana ya hili swali? Mungu alitaka maelezo, alitaka ufafanuzi, siyo kwamba hakujua kwamba Adam amekula au hakula tunda, alijua ila alimpatia nafasi ya kujieleza, kutoa mawazo yake juu ya tukio hilo.

S a s a  
k a m a  
M u m b a  
anatoa nafasi  
tujieleze sisi  
ni akina nani hata tuwazuie  
wengine? Hoja hupingwa kwa hoja,  
utafiti hupingwa kwa utafiti!

Juma lililopita Rais Samia Suluhu Hassan alipokea taarifa ya kikosi kazi cha kukusanya maoni juu ya mchakato wa katiba. Baada ya kuisikiliza taarifa ya wajumbe na mapendekezo yao naye akatoa mtazamo wake.

Baadaye, Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), John Mnyika, naye ataoa maelezo yake au uchambuzi wake wenye hoja kadhaa kuhusu kuwepo kwa kile alichokitaja kuwa ni upungufu katika taarifa ya kikosi kazi hicho.

Baadaye Mnyika, alipata wasaa wa kutoa mapendekezo yake ya kile alichooona kingefaa kufanywa. Kitendo ambacho ni haki yake kama raia, lakini zaidi kama kiongozi wa chama cha upinzani.

Baada ya uchambuzi wake huo, kikaibuka kikundi kingine kilichojitambulisha kama umoja wa vyama vya 'upinzani' kikimpinga Mnyika kwa kuipinga na kuichambua taarifa ya kikosi kazi.

Ukweli ni kwamba "muungano" huo unayo haki ya kupinga hoja za Mnyika ili siyo kumnyamazisha kana kwamba hana haki ya kuichambua taarifa ya kikosi kazi na kuonesha udhaifu wake.

Kama Mnyika alivyodadavua hoja za kikosi kazi, vivyo hivyo muungano huo ulitakiwa kudadavua hoja za Mnyika. Kumwambia hana haki ya kupinga ni kumnyima haki yake ya kikatika.

Kabla vumbi la "muungano wa vyama" halijatua, akaibuka kiongozi wa Taasisi za Wanafunzi wa Elimu ya Juu (Tahliso), Frank Nkinda, naye akimshutumu Mnyika kwa kuipinga na kuichambua taarifa ya kikosi kazi.

Kijana huyu naye anaanguka katika mtego wa muungano wa vyama vya upinzani, wa kumzuia mtu kutoa maoni yake badala ya kupinga au kuchambua hoja zake!

Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere aliwahi kuzungumzia mwenendo wa vijana wa Karne ya 20 na kueleza kuwa taifa linahitaji vijana jeuri wanaoweza kuhoji! Leo kijana wa karne ya 21 anapinga kuhoji, ni ajabu sana.

Kitu kimoja ambacho "muungano" wa vyama na Tahliso wanasahau ni kwamba Rais Samia alisema mapendekezo ya Kikosi Kazi siyo amri kwa serikali.

Sasa endapo aliyekituma Kikosi Kazi na baadaye kuwasilisha taarifa alionesha kwamba anaweza asikubaline nayo, vipi watu wengine waziwe kuichakata?



## **Kiingereza bado kizungumkuti**

**Na Scovya MANASE**

**M**ATUMIZI ya Kiingereza, ikiwa lugha ya kufundishia sekondari, yanakwamisha ufahamu mpana na kuminya uelewa wa wanafunzi.

Uchunguzi mdogo uliofanywa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, umeonesha kuwa idadi kubwa ya wanafunzi katika shule 12 zilizohusika katika uchunguzi huo wana uelewa mdogo mno wa masuala ya mazingira, afya, elimu ya uraia na hata lugha inayotumika kufundishia masomo hayo, Kiingereza.

Taarifa iliyotolewa na chama hicho jana inaonyesha kuwa wanafunzi hao wanaotoka katika shule za kata, serikali na hata binafsi na zile zinazomilikiwa na taasisi mbalimbali, hasa za dini, wanapendelea kufundishwa kwa lugha wanayoifahamu zaidi – Kiswahili ili kuelewa zaidi kinachofundishwa.

Uchunguzi huo ulijumisha wanafunzi 305, wakiwamo wasichana 167 na wawulana 138 na kwamba idadi hiyo ilichaguliwa kama sampuli ya kufanikisha zoezi hilo.

Matokeo hayo yanadhihirisha kuwa uelewa wa wanafunzi hao katika masuala mbalimbali, unaminywa na matumizi ya lugha wasiyoelewa, ambayo kimsingi ndiyo inatumika kufundishia masomo yote katika sekondari, isipokuwa Kiswahili.

“Tungekuwa tunafundishwa kwa Kiswahili na kufanya mitihani kwa lugha hiyo, tungekuwa na ufaulu mkubwa mno na kuwa vinara wa uvumbuzi wa zana mbalimbali, lakini sasa Kiingereza kinakuwa kikwazo kwetu,” hii ni kauli iliyojirudia kwa wanafunzi wengi waliohojiwa na Tampa.

Uchunguzi huo uliodumu kwa miezi miwili, ulifanyika bila kuwahusisha walimu, na kwamba wanafunzi walikuwa wakishtukizwa kwenye makutano na kuulizwa maswali matatu ya Kiingereza rahisi na hayo hayo kuulizwa kwa



*Richard Mabala, mtezi mkubwa wa matumizi ya Kiswahili*

Kiswahili.

Miongoni mwa maswali hayo ni: Je, unaelewa nini kuhusu mabadiliko ya tabia nchi? Je, Katiba ya sasa ya Tanzania inatoa muda gani kwa rais kudumu madarakani?

Majibu ya maswali hayo kwa lugha ya Kiingereza yaliwalemea, huku wengi wakionekana kujibu vyema kwa lugha ya Kiswahili.

“Ni asilimia 27 tu ya wanafunzi hao, tena wengi wakiwa kidato cha tatu na nne ndiyo walidhihirika kujibu vyema, ingawa wengine waliulizwa kwa Kiingereza na kuomba kujibu kwa Kiswahili, hali inayoonesha, wapo wanaoelewa, ingawa kujibu kwa Kiingereza ni changamoto,” alisema Tryruckia Mfinanga, kiongozi wa uchunguzi huo.

Tryruckia alisema kuwa, uchunguzi wao umegundua kuwa sababu kubwa za wanafunzi kushindwa kukimudu vyema Kiingereza, ni kukosekana kwa vitabu vya kutosha vya kiada na ziada, walimu na hata mkazo katika kuielewa lugha hiyo kupitia mbinu mbalimbali, ikiwamo klabu za masomo yote yanayofundishwa kwa Kiingereza na pia midahalo.

Alishauri serikali kuwekeza zaidi katika mafunzo ya Kiingereza, kwa kuanzia kwa walimu na katika shule za awali, kuliko hali ilivyo sasa ambapo baadhi ya wanafunzi wanajiunga na sekondari wakiwa mbumbumbu mno wa lugha hiyo.

## **Wadaiwa sugu NHC kukiona**

**Na Tryruckia MFINANGA**

**W**ADAIWA sugu wa malimbikizo ya muda mrefu ya madeni ya kodi kwenye nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) sasa kuumbuliwa.

Hawa wataanza kutangazwa hadharani katika kampeni kabambe ya kukusanya madeni hayo yanayofikia kiasi cha Sh. bilioni 26.

Mbali na kutaja majina na kiasi wanachodaiwa, wapangaji hao pia watafikishwa mahakamani ili kuhakikisha NHC inapata haki yake kwa ajili ya maendeleo.

Meneja wa Habari na Uhusiano wa NHC, Muungano Saguye ameeleza hayo jana mbele ya waandishi wa habari jijini Dar es Salaam na kwamba wadaiwa hao sugu watapewa notisi ya kuwataka kulipa madeni yao ndani ya siku 60 tangu kuipokea.

Saguye amesema kuwa awali wapangaji ambao ni wadaiwa sugu walipewa notisi ya kuanza kulipa madeni yao, lakini mwitikio haukuwa mzuri hivyo kufanikisha kukusanya Sh. bilioni 5 tu.

Amesema kutokana na hali ya ukusanyaji wa madeni hayo kuwa ya kusuasua, shirika limeamua kuongeza nguvu ya kukusanya madeni hayo kwa wapangaji waliopo kwenye nyumba na wapangaji waliohama wanaodaiwa malimbikizo ya kodi hadi sasa.

“Wale watakaoshindwa kutekeleza ndani ya muda uliotolewa, shirika litawatangaza kwenye vyombo vya habari ili Watanzania wawafahamu watu wanaokwamisha shirika lao na tutawachukulia hatua za kisheria ikiwemo kuwafikisha mahakamani,” ameegeza.

Saguye amesema kitendo cha wapangaji hao kukimbia na madeni ya nyumba ni sawa na uhujumu ambao hautavumiliwa na kwamba shirika linaenda kuwasaka popote walipo kwa kutumia mbinu mbalimbali.

Amesema shirika linashirikiana na vyombo vingine vya dola kuhakikisha



**Nehemia Mchechu - Mkurugenzi Mkuu wa NHC**

kuwa wapangaji hao wanapatikana na wanalipa kodi zao.

NHC ilianza kuyafanyia mapitio madeni ya kodi na kuyahakiki ili kubainisha kila mdaiwa na mahali alipo na zoezi la kukusanya madeni lilianza Januari, mwaka huu.

Shirika hilo limeeleza kwamba malimbikizo hayo ya Sh. bilioni 26, yana uwezo wa kujenga nyumba nyingine 450 ambazo zitawasaidia Watanzania wengine kupata makazi kupitia NHC.

Saguye amesema kuwa shirika limebaini wapangaji wasio halali wanaoishi kwenye nyumba kinyume na utaratibu wapatao 30 na tayari wamewachukulia hatua za kisheria kwa kuwanyang'anya upangaji na kuwapatia wanaostahili.

Shirika hilo mwaka jana lilitenga Sh. bilioni 8.5 kukarabati majengo yake 350 ambapo mpaka sasa limeshaanza ukarabati wa baadhi ya majengo katika mikoa ya Kilimanjaro na Dar es Salaam.



## **Nguzo za demokrasia – I**

**K**ABLA sijaendelea kuangalia hatua nyingine ya mgawo wa madaraka, ni vyema kuongeza minofu kidogo katika dhana ya demokrasia.

Mtazamo wangu unaweza usipendwe sana na baadhi ya wasomaji, kwani una mwelekeo wa kufanya demokrasia kuwa kipimo cha ubora wa tawala.

Hii maana yake ni kama vile kupima utawala kwa viwango vya kuanzia asilimia 100 hadi zero - ya uwepo wa demokrasia. Mjadala huu utaoonyesha kwa nini demokrasia inazo sifa za kuwa kipimo cha ubora wa tawala.

Niliwahi kutaja aina za demokrasia; hii ilikuwa ni kutaja wingi wa aina za demokrasia. Hapa napenda kuzungumza kwa kifupi juu ya misingi ya demokrasia. Kwa kufanya hivyo ni sawa na kutazama demokrasia kwa uthamania.

Misingi ya demokrasia ndio huleta uzuri wa uelewa wake na kutuwezeshia kuelewa hata lugha za ulinganifu kama vile demokrasia changa na demokrasia komavu.

Katika kitabu changu “Kati ya Siasa na Amani” nimezungumzia misingi hii. Kuna utawanyiko mkubwa juu ya idadi ya misingi hiyo. Hata hivyo, mtawanyiko huo unaosababishwa na ufafanuzi unaowekwa na kila mwandishi.


Mambo yale ambayo huonekana kama misingi kwa wengine, huchukuliwa na wengine kama ufafanuzi. Katika kichwa hiki nitataja misingi saba kwa urahisi ambayo nionavyo mimi inaleta picha ya uelewa wa demokrasia.

Leo nitataja mbili kati ya hizo saba na zingine zitafuata katika makala ifuatayo.

Kwanza, kutambulika na kukubalika kwa utawala ni halali. Utawala unaopatikana kwa mchakato wa kidemokrasia, hauna maswali juu ya kutambulika na kukubalika kwamba ni halali.

Chimbuko lake ni mchakato huru, wa wazi na haki. Utawala wa jinsi hii huungia madarakani kwa ridhaa, siyo ya wengi tu, bali ya makundi yote.

Siyo uchaguzi ambao matokeo



**Katiba**

yakitangazwa tu - watu wanakuwa wamechoshana, wamechukiana, na wapinzani tele wapo mahabusu au kukimbia nchi.

Serikali inayosababisha mateso ya jinsi hiyo inajua wazi kwamba kutambulika na kukubalika kwake siyo halali na inakuwepo kwa kutumia nguvu za dola.

**Pili**, kutawala kwa kufuta sheria. Hii ni sifa muhimu sana kwani ndio hasa kigezo cha kupatikana kwa serikali halali inauyotambulika na kukubalika. Hata hivyo, uchaguzi na matokeo yake ni sehemu tu ya kudhihirika kwa utawala wa sheria.

Hata hivyo, pia kuna ukweli kwamba nyakati za uchaguzi ni miongoni mwa nyakati ambazo kuna tishio kubwa la kuvunjwa kwa sheria. Siasa kwa sehemu kubwa ni juu ya kutawala. Kwa hiyo kuingia madarakani ni njaa na kiu ya waniasia wote.

Hii ndio sababu wengi wao hutumia njia zozote, ikiwemo kuvunja sheria, ili kupata madaraka hayo na kujikusanyia nguvu.

Pamoja na umuhimu wa kutii sheria wakati wa uchaguzi, utawala wa sheria unapaswa kuwa mapigo ya moyo wa taifa. Sheria ndizo huratibisha haki na wajibu za makundi yote katika jamii.

Sheria ndio huratibisha kiasi cha uhuru wa watawala katika kutimiza wajibu wao; na wakati huohuo kulinda mipaka yao pale wanapotekeleza wajibu wao kwa mujibu wa sheria.

Kwa upande mwingine, ni sheria zinaratibisha maisha ya jamii kwa kuweka vipimo vya haki na uhuru wao. Kwa kiwango kikubwa sheria hizi zina chimbuko lake kwa jamii au wananchi.

---





**Na Evarist Chahali**  
evarist@chahali.com

## Rostam kanena, kamari ni janga

**K**ATIKA toleo lililopita la gazeti hili, kulikuwa na habari ya kurasa tatu kuhusu kauli ya mfanyabiashara maarufu Rostam Aziz juu ya “wawekezaji uchwara” hususan kutoka nchini China.

Niliguswa na mambo matatu kuhusiana na aliyooonea Rostam. Kwanza, yeye kama mmoja wa Watanzania wachache matajiri wakubwa, kuguswa na umasikini wa wengine, ni jambo linalipaswa, siyo tu kupongezwa, bali pia kuigwa na kila Mtanzania.

Kama ambavyo baadhi ya watu walivyopokea angalizo hilo kuhusu wawekezaji uchwara, ambapo baadhi waliona kama siyo tatizo kwao (pengine kwa vile haliwaathiri wao moja kwa moja), Rostam angeweza pia kupuuzia suala hilo kwa sababu halina athari kwake.

Lakini, ameguswa kwa sababu hivyo ndivyo sote tunapaswa kuwa; kuwajali wenzetu hata kama kutowajali hakutowaathiri au kuwajali hakutunufaishi.

Jambo jingine lililonigusa kutokana na alichooonea Rostam ni kubaini kwamba kumbe tatizo la Wachina kusambaza mashine za kamari limetapakaa sana, hususan maeneo ya vijijini. Cha kushangaza, kabla ya Rostam kuongelea suala hilo, sijawahi kusikia Watanzania wakizungumzia hilo.

Kwa vile mie kutosikia suala hilo hakumaanishi halijawahi kuongelewa, nilijibidiisha kutafuta mtandaoni na kuuliza watu mbalimbali, na nilijiridhisha kuwa hakuna maongezi ya kutosha kuhusiana na suala hilo.

Jambo la tatu lililonigusa na mapokeo duni ya tahadhari aliyotoa Rostam, angalau kwenye mitandao ya kijamii. Mapokeo duni kwa maana kwamba kwa watu wengi hawakuonyesha kushtushwa au hata kukasirishwa na “wawekezaji uchwara” hususan katika huo “uwekezaji”



**Rostam Aziz**

wa mashine za kamari vijijini ambazo kimsingi zinawaongezea tu umasikini wanavijiji huku zikiwapa ndoto hewa za utajiri.

Katika mjadala uliojitokeza baada ya mie kuchapisha makala iliyobeba kurasa tatu za Pambazuko zenye kauli ya Rostam, watu wengi waliilaumu serikali kwa kuruhusu “wawekezaji uchwara” kufanya shughuli zao nchini.

Kuhusu mashine za kamari vijijini, wadau wengi walidai kwamba suala zima la kutegemea kamari kubadilisha maisha ya mtu linachangiwa zaidi na ukosefu wa elimu.

Hata hivyo, huku nchi za Magharibi, kulowea kwenye kamari kunaangaliwa kwa uzito unaokaribiana na athari za uraibu wa dawa za kulevyu.

Mwisho, safu hii inatoa mwito kwa serikali kufanyia kazi kauli ya Rostam kuhusu wawekezaji feki, sambamba na kuchukua hatua stahili katika kuepusha “majanga” yanayoweza kusababishwa na kutapakaa kwa mashine za kamari hususan huko vijijini.

---

**Jacqueline Mengi anyimwa milioni 695/-****Na Mwandishi WETU**

**Z**AIDI ya Sh. milioni 695 alizoomba Jacqueline Ntuyabaliwe apewe na wasimamizi wa mirathi ya mumewe, Reginald Abraham Mengi, kwa ajili ya kile alichodai kuwa malimbikizo ya matunzo ya watoto wake, sasa hatazipata.

Hivi karibuni Jacqueline alifungua shauri mahakamani akidai kupewa kiasi cha Sh. 695,890,960 ili kulipa fidia ya gharama za kulea watoto hao; Jayden Kihoza Mengi na Ryan Saashisha Mengi waliozaliwa Oktoba Mosi, 2012.

Katika kesi aliyofungua Mahakama ya Watoto Kisutu, Dar es Salaam, Jacqueline alikuwa akiwalalamikia Abdiel Reginald Mengi (mtoto wa Mengi) pamoja na Benjamin Abraham Mengi (mdogo wa Mengi), ambao ni wasimamizi wa mirathi ya marehemu Mengi.

Hata hivyo, hukumu iliyotolewa chini ya kesi ya madai namba 50/2022 iliyosajiliwa na Jacqueline ilikataa kubariki maombi yake hao.

Katika kesi hiyo, Jacqueline alikuwa na maombi mawili makubwa; kwanza, ni malipo ya nyuma kiasi cha Sh. 401,956,480 kwa ajili ya matunzo ya watoto wake. Anadai kuwa deni hili linatokana na malipo ambayo hayakutolewa na wasimamizi wa mirathi kwa wakati, japo anadai kwa mujibu wa bajeti ya matunzo iliyokuwa inatumiwa na baba mzazi, Reginald Mengi, yalipaswa kufanyika.

Madai ya pili ni Sh. 293,934,480 alizodai ni kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya watoto kama ifuatavyo; karo ya mwaka tangu Agosti 2021 hadi Julai, 2022 (Sh. 94,392,000); karo ya mwaka tangu Agosti 2022 hadi Julai 2023 (Sh. 94,392,000); usafiri wa watoto (Sh. 24,000,000); bima ya afya ya watoto (Sh. 30,000,000); matunzo ya jumla kama chakula na mavazi (Sh. 15,000,000); na bima ya nyumba (Sh. 36,150,480).

Lakini, kupitia hukumu ya Mahakama ya Kisutu ya Agosti 22, 2022, korti hiyo

ilikataa 'kubariki' maombi haya kwa sababu tatu.

**Kwanza**, wadaiwa ni wasimamizi wa mirathi, kupitia kesi namba 39/2019, na mchakato wa kukusanya na kugawanya madeni na mali kwa warithi halali haujakamilika. Hivyo, mahakama hiyo ya watoto inaona kuwa madai yote yanapaswa kupelekwa kwenye mahakama ya mirathi.

**Pili**, mahakama ya watoto imesema kuwa deni la nyuma kiasi cha Sh. 401,956,480 kwa ajili ya matunzo ya watoto wawili halipaswi kulipwa na wasimamizi wa mirathi kwa sababu wao siyo wazazi wa damu wa watoto hao, na hawahusiki na bajeti iliyokuwa inatumiwa na baba yao.

Na tatu, kuhusu madai ya Sh. 293,934,480 kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya watoto, mahakama imewaelekeza wasimamizi wa mirathi kutoa huduma kulingana na uwezo wa kifedha walionao kwa sasa, na kwamba waendeleo na jukumu lao kisheria hadi hapo mirathi itakapofungwa rasmi na mahakama.

Jacqueline alitaka alipwe kiasi hicho cha fedha - Sh. 695,890,960 kutokana na vyanzo mbalimbali vya mali za hayati mumewe.

Vyanzo hivyo ni pamoja na Kampuni za IPP, Kituo cha Televisheni cha ITV, Radio One, EATV, Bonite Bottlers, Guardian, Nipashe, Gold Africa, M-Mining, Diamond AFR, Energy TZ, na IPP Auto Mobile.

Hata hivyo, katika utetezi wake, wakili wa walalamikiwa alidai kwamba Jacqueline anatumia mgongo wa watoto kudai fedha nyingi kwa ajili ya kupata fedha za kufanikisha mtindo wake wa maisha.

Mahakama hiyo ilieleza kwamba Jacqueline amekaidi kukutana na wasimamizi wa mirathi ili kupanga namna nzuri ya kuhakikisha maisha ya watoto wake wawili yanavyoendeshwa kwa kadri ya viwango vinavyoendana na wakati wa uhai wa baba yao.

---

## **Jacqueline Mengi anyimwa milioni 695/-**

Kwamba Jacqueline amekuwa akishirikiana na dada yake ambaye jina lake halikutajwa mahakamani, kufanya matumizi kwa ajili ya familia na kuwasilisha ankara kwa wasimamizi wa mirathi bila kushauriana, hali ambayo wasimamizi wanailalamikia kuwa inavuruga makubaliano na mtiririko wa matumizi yaliyoidhinishwa na familia.

Maisha ya watoto wa Jacqueline

Uchunguzi wa gazeti hili umebaini kuwa watoto wa Jacqueline; Jayden na Ryan waliendelea kuishi maisha kama alivyokuwepo baba yao. Kwamba wameendelea kusomesha International School of Tanganyika (IST), Dar es Salaam, huku wakipewa staili ya maisha kama walivyokuwa wakiishi na baba yao.

Gharama ya kusomesha mtoto mmoja katika shule hiyo huanzia Sh. 37,000,000 – kwa madarasa ya awali hadi Sh. 78,000,000 kwa madarasa yanayofuata kwa muda wa mwaka mmoja.

Pia watoto hao na mama yao wana walinzi wawili, wanaokuwa nao muda wote, wana bima za afya ambazo zinawaruhusu kwenda kutibiwa popote duniani na kwa muda wowote.

Imebainika kuwa watoto hao pamoja na mama yao, wanaendelea na maisha yaleyale ya kifahari, bila kuwepo mkwamo wala tofauti na wakati wa uhai wa Mengi.

Jacqueline aishi Dubai

Gazeti hili limepewa taarifa kwamba Jacqueline ameamua kuwaondoa watoto hao Tanzania na kwenda kuishi nao Dubai, ambako wameanza kusoma bila kuhusisha wasimamizi wa mirathi.

Wasimamizi wa mirathi walipotafutwa ili kuthibitisha hili, wote wawili hawakuwa tayari kuzungumza kwa maelezo kwamba ni masuala ya familia.

Pambazuko lilifika shule wanayosoma watoto hao, IST na kupata kueleza kwamba Jayden na Ryan wameombewa ruhusa ya safari, lakini mtoa taarifa hakuwa tayari kueleza ruhusa hiyo ni ya muda gani na hakuwa tayari kueleza endapo labda wameombewa uhamisho.



**Jacqueline Ntuyabaliwe**

Mmoja wa marafiki wa Jacqueline ameliambia gazeti hili kwamba ni kweli rafiki yake kwa sasa anaishi Dubai na amepata kazi ya kufanya huko, hivyo hawezi kurejea na kuishi nchini kwa sasa, labda “itokee vinginevyo.”

Akikataa kutajwa jina gazetini, amesema watoto wa Jacqueline wanasoma huko Dubai, ingawa hakuwa tayari kutaja shule wala mahali wanakoishi.

---

## Tishio uwanja wa ndege Z'Bar

Na Jabir IDRISSA

**M**GOGORO mkubwa unatishia uendeshaji wa uhakika wa shughuli za uwanja wa ndege wa kimataifa wa Zanzibar endapo hautatuliwa mapema.

Endapo hali hiyo itaachwa itokee, ajira za watumishi zaidi 600 zitakuwa shakani, huku serikali ikikosa mapato makubwa yanayotokana na uwanja huo.

Tishio hilo linafuatia kusudio la kuishtaki serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) baada ya kuridhia mkataba wa haki za kipekee kwa Kampuni ya Dnata ya Dubai.

Hapana shaka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar “hajafikiria kamwe” kubadili uamuzi wake wa kuipa mkataba kampuni hiyo yenye hadhi ya kimataifa, wa kutoa huduma kwa ndege zinazotua kwenye eneo la uwanja wa kisasa (Terminal 3) uliokamilika ujenzi wake mwaka uliopita.

“Hakuna kitu kama hicho kwenye mtizamo wa uongozi wa sasa. Uamuzi uliofanywa umetokana na hatua zilizo chukuliwa kwa mpangilio na kutokana na dhamira nzuri ya kuiongezea mapato serikali na hivyo kukuza uchumi kupitia sekta hii ya usafiri na usafirishaji kwa njia ya anga,” ndio kauli ya ofisa mwandamizi Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ya Zanzibar.

Kwa mujibu wa ofisa huyo aliyetoa sharti la kutotajwa kwa kuwa siyo msemaji rasmi wa wizara wala mamlaka, kila hatua imetekelezwa kiutaratibu na uamuzi wa serikali kusaini mkataba na Dnata, Novemba mwaka jana, haujabadilika.

Dnata wanatarajia kuanza kazi wakiwa peke yao katika uendeshaji wa kiwanja hicho ifikapo Desemba Mosi mwaka huu.

Msisitizo huu unaelezwa sasa wakati Chama cha Wahudumiaji Ndege Tanzania (Taoa) kinashikilia kupinga uamuzi huo, hususan kwa kuwa unaipa Dnata “haki ya kipekee” ya kuhudumia ndege zote zinazotua Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (AAKIA).

Toa kinadai kuwa kuipa haki



Rais Mwinyi

zote za kuhudumia AAKIA ni kukiuka sheria, kanuni na maelekezo ya Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ya Tanzania (TCAA) na Sheria ya Ushindani wa Haki.

Chama hicho kijipanga kwenda kortini kupitia kampuni ya uwakili ya B&E AKO kuhoji uhalali huo huku wakitaka TCAA iingilie kati suala hilo kwa “kuiigiza” mamlaka ya Zanzibar kusitisha uamuzi wake huo na kuruhusu majadiliano na pande zote husika kama hatua ya kushughulikia tatizo kitaratibu na kwa maslahi mapana ya nchi.

Tayari mawakili hao walimuandikia barua Mkurugenzi Mkuu wa TCAA kumjulisha kuwa madai ya wateja wao yasiipotimizwa katika watachukua hatua ya kufungua shauri litakalohusu madai ya gharama kwa kuwa “wateja wetu wameguswa sana na uamuzi wa ZAA.”

Kuanza kwa mkataba huo wa Dnata, unaziweka kando kampuni za ZAT - iliyohudumu kwa miaka mingi ikimilikiwa na Mohamed Raza, mfanyabiashara maarufu na Transworld iliyoanza biashara mwaka 2019.

## **Alikotoka Mganga Mkuu wa Serikali**

Na Mwandishi WETU

**T**ANZANIA imepata Mganga Mkuu wa Serikali mpya baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kumteua Profesa Tumaini Joseph Nagu.

Profesa Nagu ni daktari bingwa wa magonjwa ya viungo vya ndani ya mwili wa binadamu akiwa na uzoefu unaofikia miaka 20.

Uteuzi wa Profesa Nagu ulianza tangu Oktoba 19, mwaka huu.

Taratibu za kazi kwa nafasi hiyo zinaeleza kuwa Profesa Nagu atakuwa akitekeleza majukumu yake kupitia kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya.

Kazi kubwa ya Mganga Mkuu wa Serikali ni kusimamia vitengo na vitengo vya wizara ambavyo vinaongozwa na wakurugenzi na wakuu wengine wa idara husika. Kazi yake pia inahusu kusimamia majukumu ya waganga wakuu wa mikoa yote Tanzania.

Wakati akiteuliwa na Rais Samia, Profesa Nagu alikuwa Kaimu Mkuu wa Idara ya Tiba ya Ndani katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili. Awali aliwahi kuwa Mkuu wa Idara ya Magonjwa ya Ndani ya Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Profesa Nagu pia ni bingwa wa utafiti na matibabu ya magonjwa ya mapafu na magonjwa ya kuambukiza, pia amefanya kazi akiwa mshauri mkuu wa ufuatiliaji na tathmini ya afya ya umma ndani na nje ya Tanzania.

Profesa Nagu anachukua nafasi iliyokuwa 'ikikaliwa' na Dkt. Aifello Sichwale ambaye taarifa ya Ikulu inaeleza atapangiwa majukumu mengine.

Profesa Nagu ana shahada ya uzamivu (Ph.D) katika Sayansi ya Tiba kutoka Taasisi ya Karolinska - Stockholm, Uswidi ambayo alipata Desemba 2017.

Mwaka 2008, alihitimu shahada ya uzamili ya udaktari wa magonjwa ya ndani ya mwili wa binadamu kutoka Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi



*Profesa Tumaini Joseph Nagu.*

***Kazi kubwa ya Mganga Mkuu wa Serikali ni kusimamia vitengo na vitengo vya wizara ambavyo vinaongozwa na wakurugenzi na wakuu wengine wa idara husika.***

Muhimbili (MUHAS), Dar es Salaam.

Pia alipata shahada ya uzamili ya kuhusu methodolojia juu ya takwimu na magonjwa kutoka Chuo Kikuu cha Brussels, Ubelgiji 2003.

Alipata shahada yake ya udaktari wa tiba kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 2002 na alifanya kazi baadaye akiwa daktari kwa miaka mingi kabla ya kuanza masomo ya uzamili.



---

**Mtanzania aibuka kidedea**

*Mrembo wa Tanzania Hadija Kanyama (namba 9 ya utambulisho) ametwaa taji la urembo la dunia kwa viziwi katika shindano lililofanyika Dar es Salaam na kutangazwa ushindi huo na jopo la majaji 8 wakiongozwa na Rais wa Mashindano Urembo kwa Viziwi Duniani, Baneta Ann Li kutoka nchini Marekani.*



*Waziri wa, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohammed Mchengerwa (kulia), katibu wake mkuu, Dkt. Hassan Abbas (katikati) na wakuu wengine wa serikali walishuhudia michuano hiyo.*

---

## Mwoleka: Sifa zamfuata kaburini

Na Deusededith KAHANGWA

**B**INADAMU mwenye maono, aliyegusa maisha ya watu na hata kuweka alama nzuri katika taasisi, sifa kedekeke humfuata hata baada ya kufariki dunia.

Wanaoifuatwa na sifa makaburini, bila kujali muda walioondoka juu ya uso wa dunia wapo wengi; wapo wanasiasa, walimu, wanamuziki, maaskofu, wachungaji, wafanyabiashara, waandishi wa habari na watu wa kada mbalimbali.

Kanisa Katoliki lina mmoja – miongonio mwa wengi, wa watu walioacha maono na walioweka misingi ya kukumbukwa hadi leo, miaka 10 baada ya kufariki dunia. Mtu huyo ni Askofu Christopher Mwoleka (1927-2002) wa Jimbo la Rulenge (wakati huo), lililoko Kaskazini Magharibi mwa Tanzania. Alifariki dunia Oktoba 16, 2002, akiwa na miaka 75.

Alizikwa Oktoba 19, 2002, huko Rulenge, Wilaya ya Ngara, mkoani Kagera.

Askofu Mwoleka alikuwa maarufu Afrika na duniani kwa sababu ya mafundisho yake kuhusu Ujamaa na Utatu Mtakatifu, na jinsi alivyoyatafsiri kwa vitendo alichokiamini kupitia jumua ndogo ndogo za Kikristo.

Mwoleka alifanikiwa kuwashawishi maaskofu wenzake katika ukanda wa Afrika Mshariki (Amecea - Association of Member Episcopal Conferences of Eastern Africa) kubebebera ya jumua hizo kuwa kipaumbele chake katika kazi ya uenjlilishaji.

Mwoleka aliandika vitabu vingi kuhusu hoja alyoisimamia, lakini andiko lake lililonukuliwa zaidi na kuchapishwa kama sura mojawapo katika vitabu kadhaa duniani, ni makala yake yenye kichwa cha maneno “Trinity and Community.”

Katika andiko hili, Mwoleka anasema kuwa, “Mungu hakufunua fumbo la Utatu Mtakatifu kama “chemshabongo” ya kujadiliwa miaka nenda rudi.

Badala yake, anasema kuwa Mungu amefunua fumbo hili kusudi tupate mfano



Askofu Mwoleka

wa namna ya kuishi tukiwa wajamaa, kama ambavyo Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu, wanaishi kijamaa, kwa upendo, na katika umoja wa kudumu.”

Kwa maoni yake, siasa ya vijiji vya ujamaa vilivyoanzishwa na Mwalimu Nyerere, ni mazingira mwafaka kwa Kanisa kuweka katika vitendo fundisho la Utatu Mtakatifu kwa kuunda jumua hivyo katika vijiji.

Mwoleka alishiriki kuanzisha na kuishi katika kijiji kimojawapo cha ujamaa kilichoitwa Nyabihanga, huko Ngara.

Mfumo wa jumua hizo sasa umekuwa ni sehemu rasmi ya Muundo wa Parokia zote Katoliki.

Hata makanisa ya Kipentekoste sasa yameiga mfumo huu na kuufanya sehemu ya muundo wa uongozi wao.

Mwaka 1975, Mwoleka akiwa Roma, alitoa hotuba kwa niaba ya timu iliyotoka Afrika Mashariki na kukosoa “mfumo kasisi”, yaani “clericalism.”

Kwa mujibu wa Mwoleka mfumo kasisi ni mfumo unaotoa picha kwamba, ukitaja Kanisa maana yake ni “makasisi”, yaani mapadre, maaskofu na makardinali, pasipokujumuisha walei. Aidha, ni mfumo ambao unawabagua wanawake katika nafasi ya daraja la upadre.



---

**Mtoto wa Museveni ‘pasua kichwa’****Na Shabaan LULELA**

**M**UHOOZI Kainerugaba, mtoto wa kiume wa Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, hatimaye amekianika kwa umma kile alichokuwa akikizungumza kwa “kuzunguka-zunguka;” kutaka kuongoza nchi hiyo baada ya baba yake.

Pamoja na kwamba haeleweki lini Rais Museveni ataondoka madarakani, lakini mtoto wake huyo, ambaye ni mwanajeshi wa cheo cha juu - jenerali, anataka kumrithi kwa udi na uvumba.

Rais Museveni (78) amekuwa madarakani kwa zaidi ya miaka 36 na hatarajii kuondoka kwa kuwa amendelea kubadili katiba ili kumruhusu kuwepo Ikulu ya nchi hiyo. Alichukua madaraka ya kuongoza Uganda kijeshi baada ya mapinduzi mwaka 1986.

Wiki iliyopita, Jenerali Muhoozi (48) aliandika katika ukurasa rasmi wa Twitter kwamba anatamani kumpa zawadi mahsusi mama yake mzazi, Janet.

Akaandika; zawadi ambayo ninaweza kumpa mama yangu mpendwa ni kuwa Rais wa Uganda! Bila shaka nitafanya hivyo!”

Pamoja na kwamba amekuwa akikanusha taarifa kwamba anajiandaa kumrithi baba yake, lakini kuna kila dalili za Muhoozi kutamani kuwa kiongozi wa juu wa nchi hiyo ya Afrika Mashariki.

Hivi karibuni, Muhoozi aliyekuwa kamanda wa kikosi maalum vya ulinzi wa baba yake, alipandishwa cheo na kufikia ujenerali, hatua ambayo ilipigiwa “kelele” na baadhi ya watu, hasa wanasiasa na wanaharakati.

Wengi wanaamini kuwa Rais Museveni anamuandaa mwanawe kuwa kiongozi kwa kuwa “haamini” mtu mwingine anayeweza kuongoza Uganda.

Muhoozi amekuwa bingwa wa kuandika ujumbe mbalimbali kwenye mtandao wa Twitter, anafananishwa na aliyekuwa Rais wa Marekani, Donald Trump, ambaye alikuwa bingwa wa kuandika ujumbe kupitia mtandao huo.

**Jenerali Muhoozi**

Trump aligeuza mtandao huo kuwa sehemu rasmi ya kuwasiliana na dunia, ingawa idara za usalama za nchi hiyo zilimzuia bila mafanikio, hadi Kampuni ya Twitter ilipomfungia maisha.

Kutokana na kuandika masuala mengine nyeti katika Twitter, Rais Museveni alimzuia Muhoozi kujihusisha na mtandao huo, lakini siku moja baadaye, mwanawe aliandika katika Twitter; “hakuna wa kunizuia kuandika kwenye Twitter, hayupi!

Rais Museveni aliwahi kumkanya Muhoozi kuwa asihusishe masuala ya kidiplomasia kati ya Uganda na nchi zningine kwani anaweza kuleta rabsha.

Maandishi ya Kainerugaba kuhusu masuala nyeti na uhusiano baina ya mataifa, mara nyingi, yamesababisha utata katika Serikali ya Uganda na uhusiano wake na mataifa mengine.

Kwa mfano, kauli zake za kuunga mkono waasi wa Tigray ilikera Serikali ya Ethiopia. Kauli zake kuhusu uvamizi wa Urusi nchini Ukraine na mapinduzi wa mwaka 2021 nchini Guinea pia ziliibua maswali mengi.

---

## Zimbabwe sasa kudhibiti VVU



*Kupima VVU*

**Z**IMBABWE imekuwa nchi ya kwanza Afrika - na ya tatu duniani kuanza matumizi ya dawa ya kuzuia Virusi Vya Ukimwi (VVU) iliyoipendekezwa na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Dawa hiyo ya sindano, Cabotegravir (CAB-LA), tayari inatumika Australia na Marekani baada ya 'kuthibitika' kuzuia maambukizi ya ugonjwa huo.

Inaelezwa kwamba dawa hiyo ya kuzuia VVU itaokoa mamilioni ya nchini Zimbabwe baada ya kuwepo ongezeko kubwa la maambukizi unaodhaniwa kuchochewa na umasikini.

Mwaka jana, Zimbabwe ilizindua mpango mkakati wa kukomesha Ukimwi ifikapo 2030 na tayari imefikia lengo linalojulikana kama 90-90-90; asilimia 90 ya watu wanaoishi na VVU, asilimia 90 wanaojitambua hali zao na asilimia 90 wanaoendelea kupata matibabu ya kurefusha maisha.

Mfumo wa huduma ya afya wa Zimbabwe unakabiliwa na matatizo makubwa, huku ugumu wa kupata huduma hizo ukikomazwa na mdiroro wa kiuchumi unaoendelea kuikabili nchi hiyo.

Tayati WHO imesema kuwa Zimbabwe kuidhinishwa kuwepo kwenye mpango wa matumizi ya dawa za kuzuia VVU kutafanya nchi hiyo kuongeza kasi ya kupambana na Ukimwi.

Dawa hiyo imeongeza matumaini ya

kupungua zaidi vifo vinavyotokana na Ukimwi na kwamba huenda kasi hiyo itazisukuma nchi zingine kuongeza kasi ya kudhibiti maambukizi.

Nyasha Sithole kutoka Mtandao wa Agenda ya Maendeleo kwa Wasichana na Wanawake Afrika (DAWA), anasema; "kuharakisha uzuiaji wa VVU kwa wasichana na wanawake vijana kunahitaji sana kwa ili kupunguza vifo."

"Ninafuraha na kujivunia uamuzi kwamba nchi yangu - Zimbabwe imeidhinisha matumizi ya CAB-LA. Hii itachangia kapu letu la zana za kuzuia VVU, kwani tulikuwa tunaoleka kubaya zaidi, hasa waathirika wakubwa wakiwa ni wasichana na wanawake," anaongeza.

"Tunaamini kuwa kila mtu anastahili kupata maelezo ambayo yana msingi wa sayansi na ukweli, na uchanganyuzi unaojikita katika uadilifu, ili wenye sifa ya kupata dawa hizo wapate," anasema.

Umoja wa Mataifa (UN) unasadia Zimbabwe kuweza kufanikisha azma yake ya kuutokomeza Ukimwi ifikapo mwaka wa 2030.

Hadi Desemba mwaka wa 2017 asilimia 87 waliokuwa wanaishi na VVU walikuwa wanafahamu hali yao kuhusu VVU ambapo kati yao hao asilimia 74 walikuwa kwenye matibabu ambapo kati yao kwenye matibabu asilimia 87 walikuwa wanatumia dawa za kupunguza makali.

## **Katiba mpya, uzalendo mpya**

**Na Mwandishi WETU**

**R**AIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, Oktoba 21, mwaka huu, alipokea ripoti ya Kikosi Kazi kilichofanya msako wa mawazo kutoka kwa wananchi kuhusu maudhui ya “Katiba Mpya na Utanzania Mpya.”

Swali mojawapo kuhusu ‘ujasiriadola’ unaofanyika kwa njia ya mchakato wa katiba mpya, na ambalo lazima lijibiwe na kikosi kazi, ni hili hapa:

Kama tukichukulia kwamba jamii ni utitiri wa watu walio huru na sawa kwa kiwango fulani, lakini pia, wakiwa ni watu wenye tofauti za kudumu katika masuala ya imani zao za kidini, kifalsafa, kimaadili na kisayansi, watu hawa wanawezaje kuishi pamoja ndani ya jamii moja yenye kuheshimu kanuni za haki na iliyo na utangamano endelevu?

Majibu kwa swali hili yatatusaidia kujua kama Watananzania wanataka katiba ya kiliberali au katiba ya kiimla, kwa sababu gani, na ipatikane kwa njia zipi.

Wakati kikosi kazi cha Rais Samia kikiwa kimekamilisha sehemu ya majukumu yake ya kusaka seti ndogo ya mawazo yanayotengeneza mwafaka wa kambi zote za kijamii, napenda kujadili majawabu ya baadhi ya maswali husika, kama yalivyotolewa na Profesa John Rawls (1921-2002) wa Marekani.

Rawls aliandika na kuchapisha vitabu kadhaa, lakini vikubwa ni viwili. Kuna “A Theory of Justice” cha mwaka 1971; na “Political Liberalism” cha mwaka 1993.

Katika maandiko yake, Rawls anapendekeza katiba ya kiliberali kwa sababu moja kubwa; uwepo wa watu wenye tofauti za kudumu katika “mifumo ya imani” zao za kidini, kifalsafa, kimaadili na kisayansi, lakini wanaopaswa kuendelea kuishi pamoja kama jumua ya kisiasa.

Kwa mujibu wa Rawls, kila “mfumo wa imani” ni seti ya matamko kadhaa yenye wafuasi, watetezi, wakosoaji na wapinzani wake. Lakini, kwa sababu za



**Prof. Rawls**

kihistoria, hii mifumo ya imani, ikiwekwa pamoja inaunda seti kuu moja yenye mikanganyiko ya kimantiki (logical contradictions).

Kwa maneno mengine, yale mapokeo ya “nchi moja, mtawala mmoja, utaiifa mmoja, imani moja” yaliyofutika tangu mkutano wa Westphalia (1648) yamepita na hayarudi tena. Badala yake, kwa mujibu wa Rawls, tunataka, na tunapaswa kutaka, “nchi moja, mtawala mmoja, utaiifa mmoja, imani mseto.”

Ni katika mazingira haya, Rawls anapendekeza kwamba, taifa lenye “imani mseto” linapaswa kuongozwa, siyo na katiba ya kiimla, bali Katiba ya kiliberali.

Katiba hii inazo sifa ifuatayo: maudhui yake yawe ni seti ndogo ya mawazo yanayotengeneza mwafaka wa kambi zote za kijamii (overlapping consensus).

Haya ni mawazo yanayoweza kukubalika kwa kambi zote kutokana na kuungwa mkono na sababu zinazokubalika kwa watu wote walio katika jumua ya kisiasa (public reasons).

# Hujambo

## Ukanushi katika njeo iliyopita

Na Dkt. Michael Mashauri

**K**ISWAHILI ni miongoni mwa lugha zinazokua kwa kasi kubwa kila siku duniani. Vyuu vikuu nje ya Afrika, vimeanza kufunza lugha hiyo adhimu. Kutokana na umuhimu wake, Pambazuko limeamua – kila wiki, kuwa njia ya kufundisha Kiswahili bure kwa yeyote anayependa.

Leo tutakuwa na darasa juu ya kiambishi cha ukanushi katika njeo iliyopita (Negation in Past Tense) ni **Ha-** kinachofuatiwa na kiambishi cha nafsi isipokuwa nafsi ya kwanza umoja inayotumia **si-** na hudondosha kiambishi cha nafsi.

Baada ya kiambishi na nafsi hufuatiwa na kiambishi **-ku-** kabla ya mziwi wa kitenzi. Nafsi ya pili umoja inaweza kutumia **hau-** au **hu-** na nafsi ya tatu umoja hudondosha kiambishi cha nafsi **-a**.

(Prefix for negation in past tense is **Ha-** which is followed by the personal prefix (or object prefix) except for first person singular which uses **si-** and drops the personal prefix.

After personal prefix, it is followed by the prefix **-ku-** before the verb root. The second person singular can use **hau-** or **hu-** and the third person singular drops the personal prefix **a-**.)

Examples			
1 <sup>st</sup> Person	Singular	Affirmative	Niliwinda wanyama (I hunted animals)
		Negative	<b>Siku</b> winda wanyama (I didn't hunt animals)
	Plural	Affirmative	Tulienda shuleni (We went to school)
		Negative	<b>Hatu</b> kunda shuleni (We didn't go to school)
2 <sup>nd</sup> Person	Singular	Affirmative	Wewe ulicheka (You laughed)
		Negative	Wewe <b>huku</b> cheka (You didn't laugh)
	Plural	Affirmative	Wewe <b>hauku</b> cheka (You didn't laugh)
		Negative	Nyinyi mlilia (You are cried)
		Affirmative	Nyinyi <b>hamku</b> lia (You did not cry)
		Negative	Nyinyi <b>hakufur</b> ahia kula ugali (He/she did not enjoy eating ugali)
3 <sup>rd</sup> Person	Singular	Affirmative	Yeye alifuraha kula ugali (He/she enjoyed eating ugali)
		Negative	Yeye <b>hakufur</b> ahia kula ugali (He/she did not enjoy eating ugali)
	Plural	Affirmative	Wao walilala hapa (They slept here)
		Negative	Wao <b>hawaku</b> lala hapa (They didn't sleep here)

Kwa nomino za ngeli nyingine, ukanushi hujitokeza kama inavyooneshwa katika jedwali chini. (For nouns from other noun classes, negation appears as shown in the table below.)

Examples			
	Singular	Affirmative	Kiti kilivunjika (A chair broke)
		Negative	Kiti <b>hakiku</b> vunjika (A chair was not broken)
	Plural	Affirmative	Viti vilivunjika (chairs broke)
		Negative	Viti <b>haviku</b> vunjika (chairs did not broke)

## **Karua bado hamtambui Ruto**



**Matha Karua**

**K**IONGOZI wa chama cha Narc Kenya, Martha Karua amesema bado hajamtambua Dkt William Ruto kuwa ni rais.

Akizungumza kwenye mahojiano na Shirika la Habari la Uingereza (BBC), Karua alisema, “Sheria imemkubali Ruto, lakini mimi bado.”

Karua ambaye alikuwa mgombea mwenza wa Raila Odinga katika Muungano wa Azimio La Umoja-One Kenya, alisisitiza kwamba, kuheshimu uamuzi wa Mahakama ya Upeo hakufai kuchukuliwa kama kutambua ushindi wa Rais Ruto.

Mbunge huyo wa zamani wa Gichugu alisema siku moja ukweli utajulikana kuhusu kilichofanyika akishikilia kuwa uchaguzi wa urais ulikumbwa na dosari zinazopaswa kurekebisha.

Akizungumza na mwandishi wa habari, Hassan Arouni wa kitengo cha Focus on Africa, Karua ameendelea kusisitiza kuwa atawasilisha kesi mahakamani kutafuta haki.

Karua alisema kwa sababu Mahakama ya Upeo ya Kenya “ilishindwa kulinda demokrasia, watawasilisha kesi katika

Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki ili kulinda na kutia nguvu taasisi na asasi za nchi”.

Alipoulizwa kuhusu uwezekano wa kufanya kazi kwa karibu na Rais Ruto, alishiria kuwa hilo halitawezekana.

“Sijakuwa serikalini kwa miaka 10, lakini sauti yangu imekuwa ikisikika. Na hivi sasa sauti yangu inaendelea kusikika zaidi,” alisema.

## **Raila: Sijachoka, sitachoka**

**M**GOMBEA urais wa Kenya katika Uchaguzi uliopita na kushindwa kwa kura chache, Raila Odinga amesema kamwe hataacha kupigania mageuzi na maendeleo ya kweli ya nchi yake.

Kiongozi huyo wa Muungano wa Azimio la Umoja One Kenya, kwa mara nyingine tena, amesema anajiandaa kukabiliana na maadui zake ambao amekuwa akidai wamemzuia kutimiza azma yake ya kuwa Rais wa Kenya.

Raila amekuwa mgombea wa urais wan chi hiyo mara tano bila kufaulu na anasema kwamba akiwa na umri wa miaka 78, hajachoka kupigania mageuzi ya utawala bora na kupalilia demokrasia na haki katika nchi hii.

“Msivunjike moyo. Kuweni imara kwa sababu mimi sijachoka. Nitawapa mwelekeo tutakaofuata wakati ukifika. Tunataka kuleta mageuzi kwa watu wetu ili Wakenya waishi maisha bora,” alisema Raila Ijumaa iliyopita akiwa kaunti yake ya nyumbani ya Siaya.

Katika uchaguzi mkuu – kwa mara tano ambazo amekuwa akigombea urais, Raila amebwagwa na marais wanne ambao ni Daniel Moi( 1997) Mwai Kabaki( 2007), Uhuru Kenyatta (2013, 2017) na Samwel Ruto( 2022).

Kila wakati akishindwa, waziri mkuu huyo wa zamani amekuwa akilaumu tume ya uchaguzi na idara ya Mahakama kwa kutumiwa kumpokonya ushindi na kushindwa kulinda haki za demokrasia.

## Sasa katiba mpya haiepukiki

Na Mchungaji Godwin CHILEWA

**I**KIWA wewe ni msomaji wa Biblia bila shaka utakuwa unakumbuka habari ya wale wanafunzi sabini waliotumwa kwenda kutangaza injili katika miji na vijiji vya Uyahudi.

Wanafunzi hawa waliporudi walimueleza Yesu kwa furaha jinsi walivyofanikiwa kufukuza mapepo na kufanya miujiza mingi. Baada ya kuwasikiliza kwa makini, Yesu aliwaonya akisema - "Msifurahi kwa kuwa pepo wanawatii, bali furahini kwa kuwa majina yenu yameandikwa mbinguni (Luka 10:20).

Ukitafakari kwa makini mazungumzo yao, utatambua kwamba wanafunzi hao hawakukosea kufurahia kwa kuona jinsi pepo walivyokuwa wakiwatii (kwa jina la Yesu). Lakini, Yesu hakuona kama hilo ni jambo la msingi.

Yeye alitaka watambue na kufurahi kwa jambo kubwa zaidi, kwamba shetani alikuwa ameangushwa toka mbinguni, na kuwa majina ya wanafunzi hao yalikuwa yameandikwa mbinguni (kwa kazi walivyofanya).

Habari hii ni ya muhimu na inafaa sana kutafakari katika kipindi hiki cha vuguvugu kubwa la kudai katiba mpya. Ni muhimu kwa sababu inatukumbusha tujitafakari kwa kina ili kutambua ni kitu gani hasa tunataka kukifanikisha katika mchakato mzima wa kudai katiba mpya, na kuchochea mabadiliko katika mfumo mzima wa utawala na uendeshaji serikali.

Tusipofanya hivyo tunaweza kufika siku ambayo tutashangilia kitu kidogo badala ya kile hasa tunachopaswa kushangilia.

Labda niweke bayana hapa kuwa binafsi naunga mkono kwa asilimia mia moja suala la kuundwa kwa katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katiba ambayo itaweka misingi imara ya utawala wa sheria, haki, na uwajibikaji.

Nina imani Watanzania wengi wanatamani jambo hili, na hata Rais mama Samia Suluhu Hassan anaamini



Rais Samia

hivyo. Nina nguvu ya kusema hivyo kwa sababu Rais Samia alikuwemo katika tume ya katiba, ambayo kusema kweli ndiyo iliyomuina kiasi cha kumfikisha hapo alipo. Kwa hiyo kwa maoni yangu katiba mpya ni jambo muhimu na la ulazima kwa wakati tulionao.

Lakini, kama nilivyogusia katika mfano wa wanafunzi wa Yesu niliueleza hapo juu, katiba mpya pekee haiwezi kumaliza matatizo ya uongozi na uwajibikaji nchini kwetu kama viongozi wetu na Watanzania wote kwa ujumla wataendelea kuwa na mtazamo au tabia waliyonayo sasa.

Tabia ya kutojali utu, kuvunja sheria bila woga, kutothamini dhamana wanayopewa na wananchi, kujiona miungu watu, na kutojali kujenga heshima inayodumu kizazi na kizazi (legacy). Yamkini hata kama katiba mpya ikishuka to

Kama hunielewi hebu fikiria nguvu ya katiba ya Marekani. Katiba iliyoundwa zaidi ya miaka 200 iliyopita na kufanya kazi nzuri ya kulinda uhuru na ustawi wa taifa hilo kwa miaka mingi.

Lakini alipoingia madarakani Rais Donald Trump katiba hiyo hiyo ilianza

## **Sasa katiba mpya haipekukiki**

*Inatoka Uk. 21*

kuonekana kama haina maana. Trump aliisigina katiba ile ile kwa kurejesha ubahuzi wa rangi kwa nguvu, kuifanya familia yake sehemu ya utawala (kama ufalme), kusambaratisha umoja wa kitaifa, na hata kujaribu kuvuruga uchaguzi mkuu ili aendelee kubaki madarakani. Katiba ilikuwepo, ileile ya miaka yote, lakini kiongozi huyu hakujali.

Hili pia tumeliona nchini mwetu. Wakati wa utawala wa marehem John Pombe Magufuli (Mwenyezi Mungu amrehemu) siyo kwamba sheria hazikuwepo kabisa la! Zilikuwepo lakini kiongozi huyo hakutaka kuzifuata wala hakutaka kuwa chini ya sheria.

Alijiona yeye ndiyo sheria. Kwa hiyo kiongozi huyu alivunja kila sheria aliyotaka kuivunja, alibomoa kila kanuni iliyombana, na kukanyaga kila utaratibu aliouchukua, na hakuna aliyethubutu kumzuia. Sidhani kama kuna mtu anaweza kupinga nikisema kuwa “hata ingekuwepo katiba mpya tunayotamani ipatikane, bado hayati Magufuli angeweza kufanya yale yale na au makubwa zaidi ya havyo bila kuzuilwa. Nani aliyekuwa na ubavu wa kumfunga paka kengele?”

Siyo hivyo tu, lakini pia zipo sheria nyingine muhimu zinazoendelea kupuuzwa hata na watumishi wadogo wa serikali wasio na nguvu yoyote.

Kwa mfano, sheria inatamka wazi kuwa Jeshi la Polisi linaruhusiwa kumuweka rumande mtuhumiwa kwa saa 24 na baada ya hapo linatakiwa kumpeleka mahakamani au kumuachia huru. Lakini mara ngapi tumeona polisi wakimshikilia mtuhumiwa kwa siku zaidi ya tano bila kumpeleka mahakamani?

Ni watu wangapi wamewahi kukamatwa na kupekuliwa bila sheria na taratibu kufuatwa? Tena siyo kwa amri ya RPC wala OCD, bali askari wa vyeo vya chini tu wasiokuwa na nidhamu?

Ninachotaka kusema ni kwamba katiba imara bila wananchi imara ni kazi bure. Ili katiba au sheria yoyote ifanye kazi ni lazima viongozi na raia wote wakubali

kujiweka chini ya utawala wa sheria, na kutii. Yamkini kama wananchi wa Marekani wasingekuwa wanajua wajibu wao, na kuzoezwa kuilinda na kuitetea katiba yao bila shaka rais mstaafu Donald Trump angeweza kupora uchaguzi na kubaki madarakani. Lakini kwa kuwa raia wa Marekani wanajitambua, wanajua haki na wajibu wao kwa taifa lao, waliweza kumdhhibiti kiongozi huyo na kuiokoa katiba yao..

Kumbe nini kifanyike? Kwanza mchakato wa kudai katiba mpya ni lazima uendelee mpaka katiba inayohitajika itakapopatikana. Hii ni kiu ya wananchi, na kwa maoni yangu naamini watanania wanayo haki ya kuipata. Katiba hii italiokoa taifa na kulifikisha katika kiwango cha juu katika kulinda uhuru, haki na demokrasia.

Lakini ili katiba hiyo iweze kufanikisha malengo yake, ni lazima watanania wote wabadilike kifikra. Kila mtanzania awe na mtazamo mpya unaoendana na malengo ya katiba mpya, ambayo ni kusunamia haki, umoja, amani na usitawi wa Watanzania.

Mabadiliko ya kifikra na mtazamo yanaweza kufikiwa endapo jitihada za makusudi zitafanywa na kila mtu kuanzia viongozi wa dini, viongozi wa vyama vya siasa, walimu, wana harakati kuwaelimisha watanania mambo ya msingi kuhusu utaiifa wao.

Mambo hayo ni pamoja na; wananchi kutambua haki zao za msingi ki sheria, na namna ya kuzipata, na au kuzidai pale wanapodhulumiwa. Tatizo kubwa lililopo sasa ni uelewa mdogo walio nao watu wengi katika masuala ya sheria.

Hili ndilo linalofanya hata pale mtu anapoporwa haki yake ya msingi hajui aanzie wapi kujitetea au kudai haki yake. Kama ujinga huu wa kutojua haki za msingi ukiachwa kuendelea watanania wataendelea kunyanyaswa hata kama tukipata katiba mpya. Ni lazima wananchi waelimishwe haki zao, na waamue kusimama kuzitetea.

*Itaendelea*



## Simba inakwama wapi?

**S**IMBA imekosa kasi na kupunguza njaa ya kutafuta mabao katika michezo mitatu iliyopita, suala lililochangia kwa kiasi kikubwa kupoteza dhidi ya Azam FC.

Simba ilipoteza mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu ilipokuwa wageni wa Azam FC kwenye Uwanja wa Mkapa, Dar es Salaam, juzi, bao la ufundi la mshambuliaji Prince Dube lilimaliza mechi.

Lakini licha ya kuruhusu bao hilo, Simba ilipiga shuti moja pekee langoni, jambo ambalo linaonekana kuota mizizi, baada ya kupiga mashuti mawili langoni kwenye mchezo wa nyuma dhidi ya Yanga.

Katika michezo mitatu iliyopita ya Simba chini ya kocha Juma Mgunda imefunga mabao mawili, wakati ikiizima Primeiro De Agosto kwa bao 1-0 kwenye Uwanja wa Mkapa, kabla ya sare ya 1-1 na Yanga na juzi kuambulia kipigo mbele ya Azam.

Mgunda alitakiwa kushituka mapema kuanzia mchezo dhidi ya De Agosto, ilipoibuka na ushindi wa bao 1-0 kwa mara ya kwanza tangu kocha huyo wa zamani wa Coastal Union apewe majukumu ya kukaimu ukocha mkuu.

Baada ya mchezo dhidi ya Yanga, Mgunda alisema kulikuwa na makosa katika safu ya ushambuliaji, akiahidi kulifanyia kazi, lakini lilijirudia juzi dhidi ya Azam FC.

“Tulipata tabu ya kupiga langoni, tulicheza na timu nzuri ambayo ilifanya kila njia kutuzuia tusiwadhuru, lakini bado tulitakiwa kufanya zaidi, nadhani ni suala la kurekebisha,” alisema Mgunda baada ya mchezo dhidi ya Yanga.

Shuti pekee katika mchezo huo lililolenga lango lilipigwa na Clatous Chama, ikiwa ni baada ya dakika za kucheza, huku Azam ikionekana kupiga mashuti kadhaa na kupata bao la ushindi.

Kocha Mgunda alisema: “Tulitakiwa kuongeza kasi katika ushambuliaji, hii ndiyo maana tulianza na washambuliaji wawili (Moses Phiri na Habib Kyombo),



Kocha Simba- Juma Mgunda

lakini bado kulikuwa na nafasi hazikutumika ipasavyo.”

Akizungumzia mchezo dhidi ya Azam FC, mmoja wa shabiki wa Simba na mchezaji wa zamani wa Miembeni ya Zanzibar, Erick Semsella alisema anaiona timu hiyo kama iliyoshuka morali katika michezo mitatu iliyopita.

Alisema katika mchezo dhidi ya Azam FC ndipo tatizo hilo lilipokuwa kubwa zaidi, huku akikataa kuwa kukosekana kwa nyota wake wachache kulichangia kipigo chao.

“Simba ilitcheza na Yanga, ilipiga mashuti mawili, shukrani ni kwamba moja lilizaa bao, lakini dhidi ya Azam FC iliichukua Simba zaidi ya saa nzima kuhakikisha inapiga golini.

**Mwanasporti**

# PICHA KUBWA



*Nyani wa bluu ambao wanapatikana Tanzania, hasa maeneo ya Ziwa Manyara, wanatajwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Sayansi na Utamaduni (Unesco) kwamba wako katika hatari ya kutoweka kutokana na kuangamizwa kwa misitu ambamo ni makazi yao makuu. Shirika hilo linahimiza nchi waliomo kuwahifadhi wanyama hao wachache kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vijavyo. (Picha ya mtandao)*

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi na Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

